

*Sheria Ndodo za Ushuru wa (Magulio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 410 la tarehe 18/09/2015

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

(SURA NA. 290)

---

**SHERIA NDOGO**

---

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 (2)*

---

SHERIA NDOGO ZA USHURU WA (MAGULIO, MASOKO NA MINADA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA, 2015

Jina na  
mwanzo wa  
kutumika

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndodo za Ushuru wa (Magulio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba za mwaka, 2015 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la  
matumizi

2. Sheria Ndodo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

Tafsiri

3. Katika sheria hizi isipokuwa itakapoeleza vinginevyo:-

“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeoyote wa Halmashauri aliyyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndodo hizi;

“Chombo cha usafiri” Maana yake ni gari la abiria, gari la mizigo, Pikipiki na kitu chochote kinachotumika kupeleka bidhaa katika Gulio, au Mnada kwa ajili ya kufanya biashara;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chemba;

“Kubinafsisha” maana yake ni uendeshaji wa Magulio na Minada kwa kutumia watu binafsi, Kampuni, Taasisi au shirika kwa niaba ya Halmashauri;

“Magulio, Masoko na Minada” maana yake ni maeneo maalum yaliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri ya Wilaya au Serikali ya kijiji kwa ajili ya wafanyabiashara kununua au kuuza mazao ya chakula, biashara, mifugo na bidhaa za viwandani;

*Sheria Ndogo za Ushuru wa (Magilio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba*

---

*Tanganzo la Serikali Na. 410 (linaendelea)*

“Mamlaka inayohusika” Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya, kamati ya maendeleo ya kata au serikali ya kijiji;

“Mifugo” Maana yake ni ng’ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe;

“Wakala” maana yake ni mtu, kampuni, shirika au taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kutekeleza jambo lolote chini ya Sheria Ndogo hizi.

Maeneo ya Magilio,  
masoko na minada

4. Halmashauri ya Wilaya itakuwa na uwezo wa kutenga maeneo kwa ajili ya magilio, masoko na minada kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Ulipaji wa ushuru na vibali

5.- (1) Halmashauri itatoza ushuru wa magilio, soko na minada ama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara wa mifugo kwenye magilio, masoko au minada kuhakikisha kuwa amepata kibali cha kuuza mifugo toka Halmashauri ya Kijiji husika au kwa Afisa Muidhiniwa kabla ya kuuza mifugo.

(3) Mmiliki yejote wa chombo cha usafiri atakayeingiza chombo hicho katika eneo la gulio, soko au mnada atawajibika kulipa ushuru wa chombo cha usafiri kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(4) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara kwenye magilio, masoko na minada kuhakikisha kuwa amesajiliwa na Halmashauri kufanya biashara husika.

(5) Mifugo itasafirishwa nje ya Halmashauri kwa msafirishaji kupewa kibali maalum cha kusafirisha mifugo kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa wakala

6. Halmashauri inaweza kumteua mtu binafsi, kampuni, asasi au Taasisi kwa ajili ya kukusanya ushuru kwenye magilio, masoko na minada ambaye majukumu yake yatakuwa:-

- (a) kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri;
- (b) kutoa maelekezo na maagizo juu ya usafi na hifadhi ya mazingira na namna ya kuendesha shughuli za gulio/mnada au soko kulingana na maagizo ya Halmashauri;

*Sheria Ndodo za Ushuru wa (Magilio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba*

---

*Tanganzo la Serikali Na. 410 (linaendelea)*

- (c) kuendesha na kudhibiti gulio/mnada au soko kulingana na Sheria Ndodo hizi pamoja na maagizo atakayopewa na Halmashauri ya Wilaya kwa nyakati tofauti;
- (d) wakala atawekeana mkataba maalum na Halmashauri ya Wilaya kwa kadri watakavyokubaliana.

Jukumu la  
Afisa  
Muidhiniwa

7. Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa kufika kwenye magilio,minada au soko wakati wa biashara kukagua utekelezaji wa Sheria Ndodo hizi.

Makosa na  
adabu

8. Mtu yejote ambaye:-

- (a) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;
- (b) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru;
- (c) atamzuia Afisa Muidhinishwa au Wakala kutekeleza majukumu yake;
- (d) atakusanya ushuru bila idhini ya Halmashauri;
- (e) afisa Muidhinishwa au Wakala atakusanya ushuru kwa kiwango ambacho ni tofauti na kilichoidhinishwa katika Sheria Ndodo hizi,

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopunguwa shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichoziidie miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Muda wa  
kufungua na  
kufunga  
magilio,  
masoko na  
minada

9. Kila gulio, soko na mnada utaanza shughuli zake kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 10.30 jioni au kadri itakavyopangwa na Halmashauri.

*Sheria Ndogo za Ushuru wa (Magilio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya  
Wilaya ya Chemba*

---

*Tangazo la Serikali Na. 410 (linaendelea)*

JEDWALI LA KWANZA

USHURU WA BIDHAA KWENYE MASOKO MAGULIO NA MINADA

S/N	AINA YA BIDHAA	KIWANGO CHA USHURU
1.	Biashara ya nguo za mitumba	Tsh. 3,000 kwa siku
2.	Biashara ya nguo za madukani	Tshs .3,000 kwa siku
3.	Biashara ya viatu vya mitumba	Tshs. 3,000 kwa siku
4	Biashara ya viatu vya madukani	Tshs. 3,000 kwa siku
5	Biashara ya Mama lishe	Tshs. 500 kwa siku
6	Biashara ya vileo	Tshs. 5,000 kwa siku
7	Biashara ya kuuza nyama	Tsh. 2,000 kwa siku
8	Michezo mbalimbali katika soko	Tshs. 2,000 kwa siku
9	Biashara ya bidhaa za urembo	Tshs. 2,000 kwa siku
10	Biashara ya vyombo vya ndani	Tshs. 2,000 kwa siku
11	Biashara ya samani mbalimbali	Tshs. 2,000 kwa siku
12	Biashara ya mazao	3% ya bei ya soko kwa kila gunia
13	Samaki	Tshs. 1,000 kwa siku
14	Vibanda au maduka	Tshs. 1,000 kwa siku

JEDWALI LA PILI  
USHURU WA KUUZA MIFUGO

S/N	AINA YA MFUGO	KIWANGO CHA USHURU
1	Ng'ombe	Tshs. 5,000 kwa Ng'ombe mmoja
2	Mbuzi	Tshs. 1,500 kwa Mbuzi mmoja
3	Kondoo/Nguruwe/Punda	Tshs. 1,500 kwa Kondoo/Nguruwe/Punda

JEDWALI LA TATU

USHURU WA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA

S/N	AINA YA KIFAA CHA USAFIRI	KIWANGO CHA USHURU
1	Gari dogo la abiria	Tshs. 500 kwa siku
2	Gari kubwa la abiria	Tshs. 1,500 kwa siku
3	Gari dogo la mizigo	Tshs. 1,000 kwa siku
4	Gari kubwa la mizigo	Tshs. 2,000 kwa siku
5	Taxi	Tshs. 1,000 kwa siku
6	Pikipiki	Tshs. 500 kwa siku
7	Kifaa kingine cha usafiri	Tshs. 500 kwa siku

*Sheria Ndogo za Ushuru wa (Magilio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya  
Wilaya ya Chemba*

*Tangazo la Serikali Na. 410 (linaendelea)*

JEDWALI LA NNE  
VIWANGO VYA ADA YA VIBALI VYA KUUZA MIFUGO

AINA YA MIFUGO	KIWANGO CHA ADA YA KIBALI
Ng'ombe/Nguruwe	Shilingi 2,000/= kwa kila ng`ombe/Nguruwe mmoja
Punda	Shilingi 1,000/=kwa kila pundu mmoja
Mbuzi/Kondoo	Shilingi 1,000/= kwa kila mbuzi/kondoo mmoja
Aina nyingine ya mifugo ambayo haikutajwa	Shilingi Shilingi 500/= kwa kila mfugo mmoja

JEDWALI LA TANO  
MAENEKO YALIPO MAGULIO, MASOKO NA MINADA

NA	JINA LA MNADA/GULIO/SOKO
1	KELEMA
2	SOYA
3	KINYAMSHINDO
4	KELEMA MAZIWANI
5	MONDO
6	GWANDI
7	SANZAWA
8	TAKWA
9	KWAMTORO
10	LALTA
11	MAZIWA
12	BABAYU
13	MRIJO CHINI/OLBOROTI
14	TANDALA
15	ITOLWA
16	GOIMA
17	SONGOLO
18	CHURUKU
19	HANDA
20	MPENDO
21	MAGAMBUA
22	FARKWA
23	TUMBAKOSE
24	MLONGIA
25	KIDOKA
26	MACHIGA
27	OVODA
28	LAHODA
29	MWAIKISABE
30	MASOKO, MAGULIO NA MINADA MENGINE YATAKAYOTENGWA NA HALMASHAURI (W) KWA AJILI YA KUUZA/KUNUNUA BIDHAA

*Sheria Ndogo za Ushuru wa (Magilio, Masoko na Minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba*

---

*Tanganzo la Serikali Na. 410 (linaendelea)*

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba uliofanyika tarehe 25 mwezi 04 mwaka 2014, Muhtasari Na. 11/2013/2014 mbele ya:-

DR. WILLIAM D. MAFWERE,  
*Mkurugenzi Mtendaji*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Chemba*

MHE. RAJABU,  
*Mwenyekiti wa*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Chemba*  
NAKUBALI,

Dodoma,  
8 Julai, 2015

MIZENGO PETER PINDA (MB.),  
*Waziri Mkuu*